MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Cheche za Fikra

JUZUU 9 TOLEO 35

APRILI 15, 2009

KIJARIDA CHA BURE— UKISHASOMA MPE MWINGINE—USIBANIE!

VITA DHIVI YA UFISADI

MPENDAZOE ATOA WITO 2010

NI MABADILIKO TU!



Benjamin. G. Mwalukasa
Mhariri



Na. Fred Katunzi

Watanzania wametakiwa kuunganisha nguvu zao na nia za na kutumia uchaguzi mkuu ujao wa 2010 kuwang'oa mafisadi na hatima kurudisha utawala wa sheria nchini pamoja na uongozi uliobora kama kweli wanataka kuleta maendeleo ya kweli nchini. Wito huo umetolewa na Mbunge wa Kishapu Mhe. Fred Mpendazoe Tungu katika waraka wake ambao ndani yake amesema kuwa kwa kuwang'oa mafisadi Watanzania hawana cha kupoteza isipokuwa "umaskini wetu".

Bw. Mpendazoe ambaye ametokea kuwa miongoni mwa kundi la wabunge wa chama tawala ambao hawaoni haya wala kupatwa na kigugumizi katika kuuita ufisadi kwa jina lake amesema kuwa kwa muda mrefu Watanzania wamekaa pembeni wakiangalia maadili ya uongozi na miiko ya uongozi ikivunjwa huku vitendo vya kifisadi vikiendelea kama vile havina matokeo yake.



Siku Kikwete alipokabidhiwa Uenyekiti wa CCM na Mkapa

"miiko ya uongozi nchini wetu Tanzania inaisha ndiyo maana viongozi wengi wanataka kutawala badala ya kuongoza, na hivyo kukumbwa na tuhuma nyingi." Amesema Bw. Mpendazoe.

Akifafanua hali halisi ya kisiasa nchini jinsi anavyoiona Mbunge

Kijarida Ulichoshika

- **Kinatoka kila Jumanne**
- **Ni cha bure kabisa!**
- **Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!**
- **Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja yoyote.**
- **Ni kijarida chako!**
- **Haki zote za kuchapa na kunakili zimerushusiwa!**

MAONI YA MHARIRI

Kutokutambua alama za nyakati ni kutokujiandaa na mabadiliiko. Alama za Nyakati tunaweza kuziona kwa kuangalia mambo yanayotokea nchini na sehemu mbalimbali duniani lakini pia kwa kuangalia kwa makusudi kabisa na kupima kitaalamu hali halisi ilivyo na kujua ni nini hasa kinachoendelea.

Mtoto anaposema kuwa anasikia homa unaweza kumpima joto kwa kutumia kiganja cha mkono wako au kuamua kumpatia kipimajoto. Kiganja kitakupa hisia kuwa kweli joto "limepanda" lakini unapotumia kipima joto unapata nafasi ya kujua limepanda kwa kiasi gani.

Kama Taifa tunaweza kusoma alama za nyakati kwa kupima joto la kisiasa na kiuchumi pamoja na la kiutawala na uongozi. **(Inaendelea Uk. 3)**

Ndani ya Toleo Hili

Mpendazoe alonga	1,2
Tahariri	1, 5
DECI: Serikali ilipe?	3
Wameuza haki yetu	4,5
DJ: Hadi kuwike?	5
Picha na Katuni	6
Maoni ya mtandao	6

"HATUNA CHA KUPOTEZA!"- MPENDAZOE

huyo ambaye mwaka jana alikuwa (Inaendelea Uk. 2) na anabakia miongoni mwa wabunge wa chache wanaopigia ukelele ufisadi nchini amesema kuwa kuna dalili ya serikali kutaka kufanya mambo pasipo kufuata sheria kama ilivyotokea kwenye suala la Dowans ambapo kampuni ya kitapeli ya Dowans Tanzania Limited ambayo ilianzishwa kwa ajili ya kuchota mabilioni ya fedha za watanzania ilitaka kuiuzia Tanesco mitambo yake ya kuzalisha umeme licha ya ukweli kwamba kama nchi ingeamua kufuata sheria mitambo hiyo ingekuwa imeshataifishwa na kuwa somo kwa "wawekezaji" wengine wanaotumia udhaifu na tamaa za viongozi wetu kujitengenezea utajiri wa haraka haraka.

"Hii dalili ya kutojali sheria ni mbaya na ya hatari sana. Sheria zipo kwa manufaa ya wananchi wote na siyo kunufaisha kikundi cha watu wachache, na upo utaratibu wa kufuata kubadilisha sheria au kufanyia marekebisho sheria kama upo ulazima wa kufanya hivyo kwa manufaa ya wananchi wote." Ameandika Mbunge huyo.

Akizungumzia suala la malumbano ya kisiasa ambayo yamekuwa yakiendelea nchini siku za hivi karibuni na ambayo yanaonesha kuendelea kushamiri licha ya kutakiwa kukomeshwa na aliyekuwa Waziri Mkuu Mzee John Malecela Bw. Mpendazoe amesema kuwa "cha haya malumbano yanayoendelea ni kupuuza **miiko ya uongozi** ambayo imesababisha rushwa nchini."

Bw. Mpendazoe amesema kuwa hakuna nchi duniani ambayo imeendelea au inataka kuendelea na ambayo haina miiko ya uongozi. "Tunakoelekea, miiko ya uongozi nchini wetu Tanzania inaisha ndiyo maana viongozi wengi wanataka kutawala badala ya kuongoza, na hivyo kukumbwa na tuhuma nyingi." Amefafanua mbunge huyo kijana wa makamo.

Akielezea jinsi gani nchi yetu imekuwa ikiingizwa katika mikataba mibovu Bw. Mpendazoe amesema kuwa sababu kubwa ya mambo haya ni kukosekana kwa uzalendo wa kweli ambao ni mapenzi ya mtu kwa nchi yake na kutoitakia mabaya.

Bw. Mpendazoe alijenga hoja kuwa "Uzalendo ungekuwepo; Wataalamu wetu wasingekubali mikataba ya aibu katika Sekta ya madini kama ilivyofanyika. Watendaji Serikalini na wataalamu wasingekubali Shirika la Reli libinafsishwe kwa mwekezaji asiye na uwezo. Aidha mgodi wa Kiwira usingebinafsishwa au kuuzwa kama "Chuma chakavu" na kwa hasara kama ilivyofanyika"

Zaidi ya yote kwa maoni yake Bw. Mpendazoe alionesha kuwa "Na ndivyo inavyotokea hapa Tanzania kwa sasa. Wageni wanaopora uchumi wetu kwenye sekta mbalimbali tunawapa heshima ya uwekezaji huku wakifilisi nchi kwa kushirikiana na Watanzania wachache waliokosa uzalendo wakiwa wamejificha kwenye vazi la maslahi ya Taifa."

Zaidi ya yote Bw. Mpendazoe alizungumzia mambo mengine yanayoendana na dhima yake hiyo kuwa ni lazima serikali iwataje na kuwachukulia hatua wamiliki wa kampuni ya Kagoda iliyochotewa kiulaghai toka Benki Kuu karibu shilingi Bilioni 40 ambazo zingeweza kutumika katika kuboresha maisha ya wananchi wanaoteseka kila siku kuzalisha na kulisukuma gurudumu la maendeleo.

Vile vile Bw. Mpendazoe ametaka serikali iliyoapa kulinda Katiba kuhakikisha kuwa karibu ya uchaguzi mkuu wa 2010 utaratibu uwekwe wa kisheria ili kuruhusu wagombea huru kwani anaamini kutofanya hivyo ni kuwanyima watu haki yao ya kimsingi ya Kikatiba.

"Kukataa kuwepo wagombea binafsi ni kupinga haki za raia, na kupinga Katiba. Ni vyema Serikali iliyoapa kuilinda katiba basi iruhusu wagombea binafsi mwaka 2010." Amefafanua.

Kutokana na mtazamo wake huo kuhusu masuala mbalimbali ya kitaifa na ambayo yanatishia kwa kiasi kikubwa nafasi ya Tanzania kupiga hatua ya haraka ya maendeleo, Mbunge huyo alisema kuwa uchaguzi ujao basi ni nafasi ya pekee kwa Watanzania kuleta kampeni ya kuleta uongozi mpya ambao utakuwa ni wa kizalendo na wenye kujali maslahi ya Taifa.

Alitoa wito kuwa kwa Watanzania kuwa "Tuungane pamoja kupinga na kutokomeza ufisadi unaoendelea nchini. Napenda kushauri na kusisitiza kwamba Umoja na mshikamano ndiyo silaha kubwa ya kupambana na dhuluma ya ufisadi unaoendelea nchini."

Aliendelea na wito wake huo kuwa "Watanzania wenzangu tuungane kupambana dhidi ya ufisadi. Hakuna cha kupoteza isipokuwa umaskini wetu. Tukiungana hakuna chochote cha kupoteza isipokuwa umaskini wetu kwa kuwa ufisadi unaoendelea kwa sasa unasababisha umaskini mkubwa kwa Watanzania. Watanzania wachache wananufaika na utajiri wa nchi hii.

Katika uchaguzi wa mwaka 2010, Watanzania tuungane pamoja dhidi ya mipango ya mafisadi ya kuendeleza dhuluma. Uchaguzi uwe ni maamuzi ya kuleta mabadiliko ya kweli kwa kila mtanzania bila kujali itikadi ya vyama.

Uwe ni uchaguzi wenye lengo la kuleta matumaini mapya kwa vijana, maamuzi thabiti ya kuleta mabadiliko kuhusu matumizi ya rasilimali za nchi yetu kwa manufaa ya wananchi wote."

Katika kumalizia barua yake ambayo unaweza kuisoma yote kwenye tovuti yetu ya Mwanakijiji.com upande wa Forum (upande wa juu kulia) Bw. Mpendazoe ameendelea kupaza sauti yake na kusema kuwa "Uchaguzi wa mwaka 2010 uwe ni uchaguzi wa kupata Viongozi wanaozingatia sheria, ni wa kweli, wenye kujali hatima ya nchi yetu na wanajua cheo ni dhamana na siyo haki yao na watoto wao."

Bw. Mpendazoe anaungana na wabunge wengine wachache ndani ya CCM ambao wanaamini kuwa mashtaka ya Kuhujumu uchumi kwa mujibu wa sheria ya Uhujumu Uchumi ya 1984 yaletwe dhidi ya wale wote waliofikishwa mahakamani na wanaotarajiwa kufikishwa hivi muda si mrefu ujao.

Katika hotuba yake aliyotoa Bungeni mwaka jana Bw. Mpendazoe alijenga hoja kuwa vitendo vilivyofanyika Benki Kuu havikuwa vya kughushu tu au kudanganya bali vilikuwa ni vya kuhujumu uchumi, na kwa vile sheria hiyo bado ipo basi ni lazima itumike. Hadi hivi sasa licha ya kuchotwa karibu shilingi trilioni moja toka Benki Kuu hakuna aliyeshtakiwa kwa kuhujumu uchumi.

Kama una maoni tofauti na yale ya Bw. Mpendazoe tuandikie: **mharirti@klhnews.**

KARIBU MWANAKIJIJI.COM

DECI: SERIKALI IMELISHINDWA LA DECI?

Na **Rashid Mahmoud**

Serikali imekiri kuwa kampuni ya kuzungusha fedha ambayo habari zake zilipamba toleo letu lililopita kweli ni ya Upatu na ya kuwa haina fedha za kutosha kuwafanya wanachama wake wote "wavune" kama wanavyotarajia.

Kukiri huko kumetolewa jana na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Mizengo Pinda (pichani)katika mkutano wake na wahariri ofisini kwake Jijini Dar jana.

Bw. Pinda amesema kuwa taarifa ambazo amezipata hadi hivi sasa zinakubaliana na maoni ya wataalamu wengi kuwa kampuni ya DECI ambayo imekuwa gumzo kubwa kwa wakazi wa sehemu mbalimbali nchini kimsingi ni kampuni ya mchezo wa upatu ambapo watu huingia na kuanza kutoa fedha zao kama mbegu wakiwa na matumaini kuwa baadaye watavuna mara nyingi zaidi.

"Hakuna cha maono wala ufunuo, DECI ni upatu tu. DECI siyo mkombozi ni ujanja ujanja ambao ambao lazima utaleta matatizo hatimaye" alisema Bw. Pinda.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu Pinda kampuni hiyo ya DECI iko matatani tayari na haina uwezo wa kuwalipa wanachama wake wote kama ikiambiwa kufanya hivyo.

Sababu kubwa iliyotolewa na Waziri Mkuu ni kuwa kwa kuangalia akaunti za DECI ni kiasi cha shilingi Bilioni moja hivi ambazo zimesalia. Hata hivyo, kiasi kinachoonekana kimeingizwa katika mzunguko wa DECI na wanachama wake ni karibu bilioni 13 huku watalaamu wengine wakiweka kiwango hicho kuwa ni makadirio ya chini kwani makadirio ya juu ni karibu bilioni 25 hivi.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu hakuna utata wowote kuwa kampuni ya DECI imevunja sheria kwa kufanya shughuli ambazo haikupewa leseni kufanya na kutokana na kiasi kikubwa kinachohusika kunafanya kuifungia mara moja kuwa ni vigumu.

Ni kutokana na hali hiyo timu imeundwa ikihusisha maafisa wa Benki Kuu, Soko la Mitaji na Dhamana na maafisa wa Polisi ili kuweza kufuatilia jinsi ya kushughulikia suala hili kwani mifano ya kuanguka kwa michezo kama hii bado iko hai na inakumbukwa sehemu mbalimbali.

Msimamo wa Cheche za Fikra bado ni ule ule kuwa shughuli za DECI hazipaswi kuendelea kama ambavyo serikali inafanya sasa ambapo badala ya kulitatua tatizo wanaliendeleza taratibu.

Ripoti ambazo tumekuwa tukizipokea tangu makala yetu itoke na licha ya matamko ya Benki Kuu na watu wa Soko la Mitaji na Dhamana bado watu wengi wanaendelea "kupanda na kuvuna" huku hali halisi ikionesha kuwa kwa kufanya hivyo tatizo la DECI linazidi kukuzwa.



Kama alivyosema Waziri Mkuu kampuni ya DECI ilivyo sasa haiwezi kuwalipa wanachama wake wote kwani kwa kuangalia akaunti zake tu haina fedha kiasi hicho.

Hata hivyo tunaamini mambo kadhaa ni ya kuzingatiwa la kwanza likiwa ni kuitaka DECI kusitisha shughuli zake mara moja. Yaani, isiendelee kuruhusu watu kuvuna wala kupanda.

Jambo la pili ni kuhakiki wanachama wake wote ambao tayari wameshapanda na kuvuna na wale ambao wanasubiri mavuno yao.

Katika kufanya hilo ni lazima kuhakiki utunzaji wa kumbukumbu za DECI unavyofanyika. Hofu yetu kama kijarida chenye kuchochea mabadiliko ya fikra tunaamini kuwa licha ya tatizo la kuzungusha fedha, taasisi hiyo haina utaratibu mzuri wa kutunza kumbukumbu.

Bila mtandao mzuri wa kompyuta na utunzaji mzuri wa nyaraka mbalimbali tunauhakika gani kuwa mtu fulani alipanda kiasi fulani na amevuna inavyotakiwa?

Kama serikali ambayo ina waajiriwa wengi na bado inahangaika na utunzaji wa kumbukumbu (wakiwemo wafanyakazi hewa) kwa taasisi binafsi kama hii ina mfumo gani wa kutunza kumbukumbu?

Kwa kuwaacha watu hawa waendelee na shughuli zao ni wazi kuwa badala ya kupunguza tatizo tunaliacha tatizo kuendelea taratibu huku michanganyo ya taarifa mbalim bali kuendelea.

Hivyo ni muhimu kwa serikali kuingilia kati na kuchukua usimamizi wa haraka wa DECI na matawi yake yote, Kubwa hata hivyo ni kukusanya nyaraka zote za kumbukumbu za wanachama na kuziweka chini ya ulinzi maalum.

Jambo hili hata hivyo ni lazima lifanywe kwa mujibu wa sheria baadaya serikali kupata amri ya Mahakama kuingilia DECI .
Pamoja na kupata taarifa zote za wanachama na viongozi wa DECI (makao makuu na matawini) serikali ihakikishe inakamata fedha zote taslimu zilizoko mikononi mwa DECI pamoja na kuzuia akaunti zake na za wamiliki wake mpaka suala hili litakapotatuliwa.

Tunatambua pasipo shaka kuwa haiwezekani kuwalipa watu wote fedha zao kutokana na fedha za DECI zilizoko benki au hata kwa kunadi mali zao zote hapa ndipo hekima ya serikali inatakiwa kwani kuna kundi kubwa la watu ambalo litajikuta haliwezi kabisa kulipwa.

Jambo la msingi na la maana ni kuwarudishia wale wote waliopanda na hawajavuna fedha zao walizopanda bila kuwalipa faida na kuona ni kiasi gani cha wanachama wa DECI wanabakia wakiidai taasisi hiyo.

Kwa wale ambao wanabakia na serikali imewahakiki na kuwathibitisha basi serikali ndiyo iwalipe fedha zao za mbegu kwa sababu katika hili uzembe hauko kwa wananchi wenye shida bali kwa serikali iliyo zembe yenye watendaji vipofu na viongozi ambao wameendelea kulala kwenye usukani.

Kama serikali yetu ingekuwa na watendaji walio makini DECI isingeweza kufika hapa ilipofikia na kutokana na ishara zilizowachanganya wananchi (kutoa leseni, kuweka ulinzi wa Polisi n.k) serikali ni mshirika wa wizi huu mkubwa na mchezo huu wa kuchezea hisia za wananchi.

Serikali ijiandae kulipa gharama za mchezo huu wa wizi uliofanywa mbele zake na kwa baraka zake!

Soma bure

HOJA YA NGUVU: WAMEUZA HAKI YETU YA MZALIWA WA KWANZA!

Na. M. M . M wanakijiji

Katika maandiko ya Biblia kuna kisa kimoja ambacho kinabakia na utata mkubwa sana kijamii na kidini. Ni kisa cha kuzaliwa kwa Yakobo. Tunachofahamu ni kuwa Yakobo alikuwa na pacha wake aitwaye Esau. Katika kisa hicho tunakutana na maneno kuwa "nimempenda Yakobo, bali Esau nimemchukia" (Malaki 1:1-3). Tunayaona hayo pia katika Waraka wa Paulo kwa Waroma 9:6-13.

Hoja yangu ya leo haihusiani na suala la "kupenda na kuchukiwa" bali hasa kile ambacho kilisimuliwa katika kisa cha kuzaliwa watoto hawa wawili katika kitabu cha Mwanzo. Kilichonigusa sana ni kuwa wakati Isaka (baba yao) anakufa Esau aliambiwa na baba yake amletee chakula akipendacho ili aweze kubarikiwa.

Kwa kutumia ujanja na kusaidiwa na mama yake (Rebecca) Yakobo alifanikiwa kuandaa chakula na kukiwaisha kwa baba yake mgonjwa ambaye alikuwa pia haoni kutokana na uzee na akiigiza sauti ya Esau kudai baraka. Licha ya kuwa na shuku mzee Isaka akaamua kutoa baraka yake ya mzaliwa wa kwanza (ambay ni Esau) kwa Yakobo (ambaye ni doto).

Wakati Esau anarudi kutoka katika mawindo yake na akiwa na njaa sana anajikuta analazimika kumuomba mdogo wake chakula ili asife njaa. Yakobo anakataa kumpa chakula ndugu yake hadi pale ndugu yake huyo atakapokubali kuuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Kutokana na kubanwa na njaa Esau akakubali kuuza haki yake hiyo na hivyo kutimiza maneno ya kinabii kuwa "mkubwa atamtumikia mdogo".

SWALI LA WIKI:

Unafikiri nini juu ya mradi wa Ponzi wa DECI? Serikali ifanye nini kuhakikisha kuwa watu hawapotezi mamlioni ya fedha zao?
Je wewe unajali?

majibu yako: **Toa majibu yako kwenye mwanakijiji.com**

Siyo lengo langu kuzungumzia suala la dini bali jambo hili limenifanya nifikirie nchi yetu ilipo leo hii na jinsi gani watawala wetu wamekuwa kama vile Esau. Kutokana na njaa zao za kila siku wamefika mahali pa kuuza haki yetu ya mzaliwa wa kwanza na matokeo yake leo hii tunatetemeka mbele ya wageni na mbele ya nchi ambazo kwa haki na kwa kila kipimo haziwezi kutufikia.

Leo hii tunatetemeka na kuwaogopa Wakenya tukiamini kuwa wameendelea kuliko sisi (katika eneo letu). Nina mashaka pia kuwa kwa kadiri utawala wetu unaendelea hivi kuna kila dalili kuwa nchi za Rwanda na Burundi, DRC, Uganda na hata Msumbiji zitapiga hatua za haraka mbele zetu huku sisi tukiandelea kutafuta kila aina ya visingizio.

Nchi karibu zote zinazotuzunguka katika eneo letu ukiondoa DRC, zimepata uhuru baada yetu! Kenya (1963), Uganda (1962), Rwanda (1962), Burundi (1962), Msumbiji (1975), Zambia (1964), na Malawi (1964).

Tulipopata uhuru tulianza kwa dhamira ya



kujenga Taifa. Tulikusudia kabisa kuwa tutachonga historia yetu kwa jinsi yetu sisi wenyewe na tulikuwa na mwelekeo wa wapi tunataka kwenda. Naamini tulikuwa mbele sana ya nchi nyingi pale tulipotangaza kuwa katika nchi yetu "kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake".

Tukipima utajiri ambao umerundikana nchini mwetu na maliasili iliyotawanyika toka mwanzo wa bahari hadi kingo za Ziwa Tanganyika na kutoka kwenye milima ya mawe izungayo Ziwa Viktoria hadi kwenye maji yameremetayo katika Pwani ya Mbaba Bay ni wazi kuwa hakuna nchi kati ya hizo zote ambayo inaweza kutufikia kwa utajiri wa asili.

Hivyo, ni vigumu kwangu kuweza kuelewa kiakili na kwa namna Fulani ninakubaliana na Rais Kikwete (japo kwa sababu tofauti) kwanini hajui imekuwaje nchi yetu kuwa ni maskini hivi!

Ninaamini kuwa mahali fulani watawala wetu wameuza haki yetu ya mzaliwa wa kwanza kuendekeza njaa zao na kuombaomba kwao kiasi kwamba wamepoteza heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wao. Matokeo yake Tanzania nchi yenye utajiri wa watu na vitu imekuwa ni ombaomba mkubwa wa "chakula" hata kujidhalilisha.

Ni kwa kiasi gani tutaendelea kuwatumikia wadogo zetu na wawekezaji feki kama kina Dowans? Ni kwa kiasi gani tutaendelea kupiga magoti kwa watu kama kina Sinclair na wawekezaji wengine tukiamini kuwa wao ndio chachu ya maendeleo yetu? Tutaendelea mpaka lini kuendelea kuchekelea wageni wanaokuja tukiamini kwamba wanakuja na zawadi za kututoa katika utumwa wa umaskini wetu?

Wakati umefika jamii ya Watanzania katika nafasi zao waamue wenyewe kuamka na kupinga utumwa huu wa kifikra na kushiriki katika mapambano ya kweli ya kurudisha heshima yetu kama Taifa la watu walio huru na sawa. Wakati umefika wa kuwapinga mafisadi na uzao wao pasipo kuwaonea haya na kuanza kuwapigia kampeni na kuwaunga mkono wale viongozi ambao kweli wanasimama kama wawakilishi wa maslahi ya taifa letu.

Tusiendelee kuwaangalia kama kwa aibu watawala ambao wanaendelea kutawala kama waliokodishwa na ambao maslahi yao ni akaunti zao za benki.

Tusikae kimya mpaka wahusika wote wa EPA wanapata adhabu ya juu kabisa kulingana na makosa yao; tusikae kimya mpaka majenereta ya Dowans hayaruhusiwi kuondolewa nchini bali kutaifishwa baada ya kuingizwa kitapeli huku yakipigiwa debe na watu mbalimbali hadi walioko Ikulu, tusikubali kukaa kimya mpaka wale wote waliohusika na Deep Green Finance (akiwemo waziri wa Mambo ya Ndani wa sasa), na wale wote waliohusika na Mwananchi

Soma Bure
hoja zenye nguvu

HOJA YA NGUVU

Gold na Merememta (wakiwemo wakuu wa Majeshi na vyombo vya usalama) wote wanafikishwa mbele ya haki.

Katika hili tunataka kuanzisha kampeni nzito kwenda kwa DPP ya kumtaka atekeleza wajibu wake wa kisheria kwa nguvu alizonazo kwa mujibu wa Katiba badala ya kujiuma uma meno na kutetemeka kwa woga mbele ya mafisadi kama anavyofanya sasa. Tusikubali mafisadi waendelee kututawala wapendavyo!

Ni kwa kufanya hivyo tu ndipo tutaonesha kwa watoto wetu na watoto wa watoto wetu kuwa haki yetu ya mzaliwa wa kwanza tumeirudisha na hatuko tayari kuipoteza tena.

Hii ni haki ambayo hatuwezi kuiweka sokoni wala kuisahau kwa wachuuzi!

MAONI YA MHARIRI

Yale yaliyotokea mwaka 2005/2006 Benki Kuu na yaliyotokea kabla yake yanatupa taarifa kuwa kwa hakika joto la "ufisadi" nchini limepanda.

Hata hivyo hatujachukua hatua za makusudi za kupima noto hilo ili kuweza kujua ni kwa kiasi gani joto hilo limepanda na ni kitu gani kifanyike kuweza kuhakikisha kuwa tunarudisha hali inayotakiwa.

Kati ya vitu vingi ambavyo watawala wetu wengi hawataki kuvikumbuka juu ya Mwalimu Nyerere (ambaye wiki anakumbukwa) ni uwezo wake wa kuwa tayari kupima nini kinaendelea nchini. Alifanya hivyo katika "Tujisahihishe" na pia katika "Miaka 10 baada ya Huru" na hata "Miaka 10 ya Azimio la Arusha". Hata wakati anaondoka katikati ya miaka themanini bado aliweza kukaa chini na kuangalia nyuma ni wapi tumetoka, tulipo na tunataka kwenda.

Kwa wanaokumbuka aliweza pia kufanya hivyo hata baada ya kutoka madarakani pale alipotoa ile hotuba ambayo tunaamini ni urithi mkubwa kwa Watanzania kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya.

Cha kusikitisha ni kuwa licha ya mabadiliko makubwa tuliyonayo leo hii siyo Rais Mwinyi wala Mkapa na hadi hivi sasa siyo Kikwete ambaye amekuwa na ujasiri wa kuangalia nyuma na kupima joto la nchi yetu na kusema ni wapi tumeenda kombo, ni nini tubadilishe na tuelekee wapi na kwa namna gani. Matokeo yake tuko kama wasafiri katika bahari ambapo nahodha na wasaidizi wake wamelala na sote

DA'JESSY: WATOTO SHEREHE MPAKA MAJOGOO?

Na. Jessica L Fundi



Nilikuwa kwenye mojawapo ya sherehe za Pasaka na kati ya vitu ambavyo vinanisumbua ni hii tabia ya wazazi na walezi kutokuwa makini na watoto wao. Ni tabia ambayo tumeizoea mno ambapo watoto wanaruhusiwa kushiriki tafrija mbalimbali hasa zile zenye muziki hadi usiku wa manane.

Hili linanifanya nikumbuka vifo vya wale watoto 19 kule Tabora katika jengo la NSSF ambapo hadi leo hii hakuna mtu anayetaka kukumbuka kwani ilikuwa ni "ajali" tu. Katika kufikiria mambo hayo nimeangalia tafrija mbalimbali hasa za siku hii ya pasaka ambapo watoto waliachwa kuselebuka hadi usiku wa manane.

Ninajiuliza hivi wazazi wako wapi? Hivi watoto hawa tunawajenga katika maadili gani au tunatarajia nani ajenge maadili ndani yao? Mambo ambao watoto hawa wanayashuhudia kwenye tafrija hizo mengine hata sisi watu wazime inabidi tuinamishe vichwa kwa aibu.

Cha kushangaza wajibu wa malezi mema kwa watoto na kuwalinda na madhara ni mkubwa, wa kwanza na wa pekee kwa mzazi yeyote yule.

Katika nchi za wenzetu ambazo zinatambua haja ya kuwalinda watoto kutoka katika vishawishi na mazingira mabaya kimaadili wazazi wa namna hiyo wananyang'anywa watoto wao!

Katika taifa letu inaonekana tumeshakubali kuwa wazazi wawalee watoto wapendavyo lakini mambo yakianza kugeuka baadaye jamii hiyo hiyo inakuwa ya kwanza kushangazwa mtoto amelelewaje?



Je tuna jinsi yoyote ambapo jamii, vilabu vya muziki, na watu wengine wenye kujali kuwa na utaratibu kuwa watoto wanapokuja kwenye sherehe za aina fulani basi mwisho wao ni hadi saa fulani na baada ya hapo mzazi anayeruhusu mtoto wake kuwa maeneo hayo yenye vishawishi vya ngono, pombe na hata matumiri haramu ya madawa basi mzazi au mlezi huyo anachukuliwa hatua?

Tutaendelea kutazama na kushuhudia kumomonyoka kwa maadili mpaka lini wakati sisi wenyewe kama wazazi na kama jamii tuna uwezo kabisa wa kuwakinga watoto wetu na vishawishi vibaya na mazingira mabaya?

Kama wazazi wanashindwa kuwalinda watoto wao katika nyumba zao na katika mitaa yao, kweli watu hao wana haki ya kuitwa wazazi au kuendelea kuwa na watoto katika himaya zao?

Ndiyo maana wakati mwingine tusipoangalia watu kama kina Madonna watakuwa wanakuja na pesa zao wakitaka kuwachukua watoto hawa kuwalea katika kile ambacho wao wanaamini ni mazingira bora! Ninaamini ipo haja ya haraka ya wazazi wa Tanzania kuunganisha nguvu zao na kuwa na msimamo mmoja wa kuishawishi serikali na wawakilishi wao na vyombo mbalimbali kulinda maslahi ya watoto siyo kwa matamko majukwaani bali kwa hatua madhubuti na za makusudi kabisa.

Vinginevyo, tujiandae kujenga taifa la watu wakorofi, wasio na maadili na ambao wanaongozwa na furahaa na hisia za raha za muda, watoto ambao hawajawahi kuambiwa "hapana".

Email: dajessy@klhnews.com

MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Picha ya Wiki



Neno "Rdevco" liliongezwa baada ya kasheshe la RDC!

PATA HABARI MOTOMOTO NA MIJADALA

http://www.mwanakijiji.com

Jiandikishe kushiriki mijadala, kupata habari, kusikiliza muziki masaa 24 na matangazo ya moja kwa moja kila mwishoni mwa juma.

Ukizungumzia habari, unatuzungumzia

KATUNI ZA WIKI



KUTOKA KWENYE MTANDAO

Wamiliki wa makampuni mengine wako mahakamani kutokana na kwamba DPP ana uthibitisho wa makampuni yote kutoka nje? Aliyemwambia DPP wetu kuwa ONUS OF PROOF katika kesi za jinai inamwangukia yeye, ni nani? Huyu kasoma kweli shule, mbabaishaji au msanii ambaye amewekwa hapo kuwahadaa Watanzania? – **Kapelwa**

Hivi hamwezi kuingilia kati kufanya mashtaka binafsi? Huyu ROSTAM mpaka aje kuomba kugombea Urais ndo mshituke? – **Fataki**

Mnataka Mrema aondoke ... haondoki mtu mpaka chama hiki kijengwe na nijue nitamwachia nani, siwezi kukiacha chama changu barabarani, haiwezekani- **Augustine Mrema**

wapo mafisadi wanajipanga kuhakikisha kuwa Rais na wabunge waliojitoa mhanga kufa kwa kupinga ufisadi nikiwemo mimi tunang'oka mwaka 2010. Nasema hivi, hang'oki mtu hapa, Kikwete ni Rais hadi 2015 na sisi wabunge tutashinda vilevile, Mungu yupo mbele yetu – **Aloyce Kimaro**

Upatu ni mifumo inayoanzishwa na wajanja duniani kote, wala haiitaji maono na ufunuo – **WM Pinda (juu ya DECI)**

Watanzania wenzangu tuungane kupambana dhidi ya ufisadi. Hakuna cha kupoteza isipokuwa umaskini wetu. Tukiungana hakuna chochote cha kupoteza isipokuwa umaskini wetu kwa kuwa ufisadi unaoendelea kwa sasa unasababisha umaskini mkubwa kwa Watanzania. Watanzania wachache wananufaika na utajiri wa nchi hii.

Uchaguzi wa mwaka 2010 uwe ni uchaguzi wa kupata Viongozi wanaozingatia sheria, ni wa kweli, wenye kujali hatima ya nchi yetu na wanajua cheo ni dhamana na siyo haki yao na watoto wao– **Mpendazoe**

When the corrupt rule, the rule is the corruption— Mwanakijiji

TOA NAKALA MOJA

Cheche za Fikra

Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi
Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha,
maoni, habari, na ushauri

Tuandikie:
mhariri@ klhnews.com

Tovuti: http://www.mwanakijiji.com

***Kanusho:** Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.*